

13- Al-Waqfu Wal-Ibtidaai – Kisimamo Na Kianzio

الْوَقْفُ وَالْإِبْتِدَاءُ

Tofauti baina ya الْوَقْفُ Al-Waqf (Kisimamo), السَّكْتُ As-Sakt (Kipumziko au Kinyamazo) na الْقَطْعُ Al-Qatw'u (Ukataji)

Istilahi hizi tatu hutumika katika fani ya kusoma Qur-aan na kila moja ina maana na kusudio lake na pahala pake pa kutumia ijapokuwa zinaonyesha kama zote zina maana moja.

الْوَقْفُ Al-Waqf - Kisimamo:

Ni kukatika sauti katika neno la Qur-aan kwa muda wa kawaida ya mtu kushusha pumzi na huku akiwa na nia ya kuendelea katika kusoma.

السَّكْتُ Al-Sakt - Kipumziko:

Ni kipumziko katika kusoma neno la Qur-aan kadiri ya haraka mbili bila ya kushusha pumzi kwa nia ya kuendelea katika kusoma.

الْقَطْعُ Al-Qatw'u Ukataji:

Ni kusimama kusoma Qur-aan kwa nia ya kumaliza kuisoma, na haijuzu kusimama isipokuwa mwisho wa Aayah au mwisho wa Suwrah; na msomaji atapotaka kurejea kusoma Qur-aan kwa mara nyengine baada ya kukata, ni juu yake kuleta الإِسْتِعَاذَةَ - Isti'aadhah.